Je wajinga wa Malecela ni wabebaji au wabebwaji?



NTHELEZI NESAA, CANADA

Kauli kuwa Chama Cha Mapinduzi katu hakitawabeba wajinga, haiwezi kupita bila kupitia kwenye darubini.

John Cigweyemisi Malecela si mtu wa kawaida katika medani za siasa za Tanzania. Malecela ni mtanzania aliyebakia aliyewahi kushika nyadhifa nyingi serikalini ukiachia kutumikia nchi kwa muda mrefu. Cheo chake cha mwisho kikubwa kisiasa ni makamu mwenyekiti wa CCM na kiserikali ni waziri mkuu.

Kumekuwa na manung'uniko kuwa CCM imekwishagawanyika kiasi cha kusubiri kufa.

Ingawa Sheikh Yahaya Hussein alitabiri mgawanyiko akaambiwa si Mungu, kosa lake lilikuwa kutabiri kitu kilichokwisha tokea. Angekuwa mkweli angetabiri kifo. Lakini asingeweza kwa kuogopa kuukata mkono umlishao. Malecela alitoa kauli kuwa CCM haiwezi kuwabeba wajinga akimaanisha mafisadi ambao bila shaka wametamalaki chamani mwake. Je mafisadi wa CCM ni wajinga au jinga ni CCM ambayo imekuwa ikiwabeba?

Je kwa kukiri kuwa kweli CCM inabeba wajinga, ndiyo mwanzo wa mgawanyiko wa wazi ukiachia mbali ile ya nyuma ihusishayo mitandao ambayo nayo kimsingi ni mama wa ufisadi unaojengwa na dhana nzima ya kujuana?

Je maneno ya Malecela ni ya kweli au kupiga chuku za siasa? Kwa anayejua historia ya nchi yetu na hasa utawala wa awamu ya nne, hatapingana na darubini kusema kuwa waziri mkuu wa zamani alibebwa na Chama chake siku kilipokaa na kumsafisha ingawa hakutakata.

Ushahidi wa wazi kwamba CCM imewahi kuwabeba wajinga wa Malecela ni kwenye sakata la wizi wa pesa ya mradi wa magari ya wanafunzi ambapo wezi wake ni makada wa CCM wanaojulikana.

Hii cha mtoto. Hivi karibuni katibu mkuu wa CCM Yusuf Makamba alinakiriwa akiwakaripia na kuwazuia wananchi kujadili kashfa mama wa kashfa ya EPA.

Kwa Makamba EPA ilikwisha kushughulikiwa siku baadhi ya wahusika walipofikishwa mahakamani. Utata zaidi ni kanusho la hivi karibuni la ikulu kuwa haikuchukua mafaili ya Kagoda kama ilivyodaiwa na Brela. Kama ikulu haikuchukua hayo mafaili, nani aliyachukua kama Brela wenyewe wanasema mafaili hayo hawana na yalichukuliwa na Ikulu?

Rejea matamshi ya Waziri wa Sheria na Katiba Mathias Chikawe, kuhusu suala la Kagoda na utagundua namna suala hili linavyopelekwa kitatautata.

Chikawe anasema kuwa serikali haiwezi kumfikisha mtu au kampuni mahakamani bila kuwa na ushahidi wa kutosha. Linganisha maneno ya Chikawe na ya mkuu wa Brela, Esteriano Mahingila kuwa nyaraka za Kagoda haziko ofisini kwake.

Ukiangalia kwa undani kilichomo ni majina ya vidagaa wawili huku mapapa wakiendelea kupeta na kukingiwa vifua? Swali linazidi kujitokeza. Je wajinga ni mafisadi au ni chama kinachowakingia kifua huku kikiendelea kukabiliwa na tishio la kuidondoshwa kwenye uchaguzi ujao?

Tuangalie zaidi nani mjinga. CCM inajulikana kuwa ina kada aitwaye Andrew Chenge mwanasheria na waziri mwandamizi wa zamani anayetuhumiwa kuwa na akaunti yenye fedha nyingi, zaidi ya shilingi 1,000,000,0 kwenye visiwa vya Jersey huko Uingereza.

Ukitazama kipato cha Chenge, unaingiwa na shaka ya wazi kuhusiana na namna alivyozipata fedha hizi.

Ajabu, tangu kashfa hii ifumke bila kukanushwa, Chenge ameendelea kuwa kada wa CCM kiasi cha hata kuteuliwa kuchunguza kashfa ya mradi wa ujenzi wa jengo la UVCCM! Chenge ameendelea kuvumiliwa na serikali ya CCM huku ikiwaaminisha watanzania kuwa inapambana na rushwa wakati ikiipamba.

Je hapa mjinga ni nani? Ukiachia mbali hao makada, kuna makampuni yanayohusishwa na ufisadi moja kwa moja kama Deep Green Finance ambayo inasemekana ni kampuni ya CCM, TICTS, Meremeta na makampuni mengine mengi.

Yote haya yanahusishwa na ufisadi ambao hayajakanusha. Lakini bado hayajafikishwa mahakamani. Je hapa mjinga ni nani? Inabidi mzee Malecela afafanue ili aeleweke. Maana anaposema CCM haiwezi kuwabeba wajinga wakati iliwabeba tangu alipoachia usukani mwalimu haelewcki vizuri.

Leo kazi ya darubini si kutoa maoni bali data ili wahusika wajue jinsi ya kujibu kama watajali au wasomaji wajiamulie. Kama tutaamua kuwa wakweli, utakuta kuwa Tanzania ni nchi pekee katika Afrika mashariki yenye wingi wa raslimali lakini iliyoko nyuma kiuchumi hata maendeleo. Ni kwanini? Kwa sababu wajinga wa Malecela wamebebwa na wanaendelea kutuibia kila uchao. Rejea ubinafsishaji uliofanywa na wajinga wa Malecela kiasi cha kuiacha nchi kwenye utata huku rais akihangaika kila uchao kutaka kurekebisha mikataba.

Madudu kama Kagoda, Richmond, IPTL, Net Group, TICTS, TRL na mengine mengi ni matokeo ya wajinga wa Malecela ambao ujingawao uliwatuma waangalie Ten Percent badala ya taifa.

Bahati mbaya chama nacho kiliangalia uwenzetu na ukereketwa, kikawaacha waiharibu nchi nzuri Tanzania! Leo hii Tanzania ni nchi pekee kusini mwa jangwa la Sahara inayolangua watu wake umeme. Kisa? Wajinga wa Malecela walipewa nafasi ya kujichumia huku wakiuchuuza na kuutoa kafara umma.

Twende kwenye nyanja nyingine muhimu ya kijamii-Elimu. Kwa sasa kuna mgongano mkubwa baina ya serikali na wanafunzi wa vyuo vya juu vya elimu. Serikali inasema haina pesa ya kuwakopesha. Lakini serikali hiyo hiyo ina pesa ya kununua mashangingi kwa ajili ya watendaji wake. Hali hii ya kipogo mpaka imemlazimisha rais Kikwete kuingilia kati kwa mujibu wa taarifa za hivi karibuni. Kama ni ujinga ni mwingi. Je wajinga wa Malecela ni wabebaji au wabebwaji?

Mwandishi wa makala ii hupotikana kwa barua pepe: nesaa1977@yahoo.com

Tuangalie zaidi nani mjinga. CCM inajulikana kuwa ina kada aitwaye Andrew Chenge mwanasheria na waziri mwandamizi wa zamani anayetuhumiwa kuwa na akaunti yenye fedha nyingi, zaidi ya shilingi 1,000,000,000 kwenye visiwa vya Jersey huko Uingereza. Ukitazama kipato cha Chenge, unaingiwa na shaka ya wazi kuhusiana na namna alivyozipata fedha hizi.

